

Kama unataka kuendelea kujitegemea



Huduma zetu sio tu kuwasaidia watu wenye shinda za macho au upofu kuendelea kujitegemea, bali pia kuhakikisha maisha yao ni rahisi, yenye usalama and ya kufurahia. Tunasaidia na:

- Upimaji wa macho na uwezo wa kuona
- Matibabu ya kikazi au Occupational therapy
- Huduma za jamii
- Huduma za nyumbani
- Mafunyo ya jinsi ya kutembea
- Mbwa wa kuongoza (Guide dogs)
- Mashauriano
- Vifaa Maluum za vipofu
- Mipango na program za wanaojitegemea
- Habari kuhusu malipo
- Usaidizi kwa wanaohudumu
- Mafunzo ya ujuzi wa kaikazi

Kujiamini

Ujuzi mpya, teknolojia mpya, marafiki wapya

Ubora/Afya

Ubora wa akili, afya ya mwili na uhodari wa mwili

Ushirikiano

Jamii, ushirika, urafiki na kusaidiana



Umoja wa vipofu WA

Kuwasiliana nasi

Kwa habari zaidi kuhusu huduma na program zetu, Nambari yetu ya simu ni: 08 9311 8202 au simu ya bure 1800 VISION

61 Kitchener Avenue
Victoria Park, Western Australia, 6100
Barua pepe: www.guidedogswa.com.au



Jarida hili limetolewa kwa usaidizi wa selikari ya mkoa wa Western Australia kupitia Idara ya Huduma kwa Walemavu

Je, una shinda ya macho?

Je, unaishi na upofu au shinda ya kupotea macho?

Hi ni habari muhimu kwako au mtu yeyote katika jamii yako ambae ana shinda ya kuona na hafaiki kwa kutumia miwani.

Kadiri watu 35,000 wa umri na nyendo mbali mbali katika mkoa wa Western Australia wana shinda za kuona au upofu.

Kwa karibu miaka 100 sasa, Shirika la Vipofu (Association for the Blind WA) limekuwa likiwasaidia vipofu na watu wenye shinda za kuona kujisaidia

Kama una shinda na upofu, jarida hili linaweza kukuangazia njia na uwezekano mpya.



Kama unataka kuendelea kujitegemea...



Michezo na mazoezi ya kimwili ni muhimu kwa ubora na afya ya kila mtu.

Tunayo nafasi na programu zenye huduma zitakazowazesha vipofu na wanaopotea macho kujitegemea na huku wakiburudika na marafiki wapya. Kwa mfano:

- Chumba chenye vifaa za mazoezi
- Programu tofauti tofauti za mazoezi
- Programu za uchoraji
- Kuchora, kuandika na kazi za mkono
- Mijadala
- Mipango ya kijamii
- Mafunzo ya usalama
- Elimu ya afya

Kama unataka kujifunza kusoma...



Shinda za macho na upofu zinaweza kusababisha shinda kwa wanaodhamini kujua yanayoendelea katika mazingira yao.

Kuipata habari uitakayo, uwezo wa kushughulikia rekodi zako au kusoma vitabu na hekaya ni muhimu sana. Tunasaidia na:

- Maktaba kubwa yenye vitabu vinavyoongea
- Maktaba yenye huduma za hali ya juu
- Teknolojia maalumu ya kutoa vitabu aina ya Braille na vitabu vilivyorekodiwa
- Usaidizi na mafunzo ya Braille
- Huduma za Elimu an mafunzo
- Vifaa maalum

Kama jamii umpendaye anendelea kupotea macho au ni kipofu...



Tunashirikiana na jamii na marafiki katika huduma zetu hili kuhakikisha watu wenye shinda za macho wanaishi maisha bora iwezekanavyo.

Huduma zetu ni kwa watu wote, kutoka wakati mtoto anaopozaliwa mpaka kwa wakonge. Huduma zetu ni kama:

- Usaidizi kwa wanaohudumia vipofu/wauguzi
- Kushirikisha wanohudumia vipofu
- Habari muhimu kwa wazazi na jamii
- Huduma muhimu za kwanza kwa waliopotea macho
- Shule za watoto wachanga (Kindergarten)
- Huduma wakati shule zimefungua kama sikukuu na mwisho wa wiki